

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
WAKALA WA VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO**



KILIMO CHA BUSTANI



Kimetayarishwa na:

**Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA)
Kampasi ya Morogoro
S.L.P. 603,
MOROGORO – TANZANIA
E-mail: litamorocamp@gmail.com**

UTANGULIZI.

Kilimo cha bustani kinahusika na uzalishaji wa mazao ya aina ya mboga, matunda, viungo na mimea ya mapambo. Kilimo hiki ni chanzo cha ajira na pato kwa wakulima na watu wengine, lakini pia mboga na matunda vinatupatia virutubisho vya kujenga, kutia nguvu na kulinda mwili.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UZALISHAJI

Ili kuzalisha kwa kiwango kikubwa, mkulima wa mazao ya bustani anapaswa kuzingatia baadhi ya mambo muhimu ikiwamo kuwa na taarifa sahihi na za kutosha kuhusu zao analolima. Mkulima anatakiwa kuwa na taarifa zote muhimu zinazohusiana na zao analotegemea kushughulika nalo. Taarifa hizi zinajumulisha upatikanaji wa mbegu bora, hali ya hewa inayopendekezwa kwa zao husika, mengine ni taarifa kuhusu magonjwa na wadudu wanaoweza kulishambulia zao hilo na namna ya kuyakabili, pamoja na uhitaji wake katika soko la ndani na la nje.

MISINGI YA UZALISHAJI

Ili mkulima aweze kuzalisha kwa tija na kwa gharama nafuu wakati huo huo akilinda afya yake na ya walaji, ni muhimu kuzalisha kwa misingi ya kilimo hai. Fanya uzalishaji wa mazao kwa kuzingatia misingi hii kuanzia kwenye mbegu kwa kutumia mbegu zilizozalishwa kwa misingi ya kilimo hai, matumizi ya mbolea hai, dawa za kudhibiti magonjwa na wadudu pamoja na uhifadhi wa

mavuno au mazao yako ghalani au katika usindikaji.

Kilimo hai ni aina ya kilimo kisichotumia madawa wala kemikali za viwandani. Bidhaa zitokanazo na kilimo hai zinaelezwa kuwa na ubora maradufu kuliko bidhaa zitokanazo na madawa na mbolea za viwandani.

ENEO NA HALI YA HEWA

Kabla mkulima hajafikiria juu ya kulima zao fulani, ni lazima ahakikishe kuwa ana eneo la kutosha kwa ajili ya mazao yake. Lakini pia ahakikishe kuwa hali ya hewa ya eneo hilo inaoana na zao analotaka kulima.

GHARAMA ZA UZALISHAJI

Jambo hili ni la msingi kwani huwezi kufanya kilimo bila kuingia katika gharama za uzalishaji. Gharama hizi ni pamoja na ununuzi wa mbegu, maandalizi ya shamba, utunzaji wa zao shambani kwa kudhibiti wadudu na magonjwa, uvunaji na upelekaji sokoni au usindikaji.

UPATIKANAJI WA SOKO

Suala la soko ni la msingi na ni la wakati wote, kuanzia kipindi cha utafutaji taarifa ya zao husika, wakati zao likiwa katika hatua ya awali ya uzalishaji na hata linapokuwa tayari kwenda sokoni. Ni muhimu kwa mkulima kutafuta soko la mazao yake ili aweze kuuza kwa bei iliyopo sokoni na ikiwa bei imeshuka kwa ghalfa bila kutarajiwa, aweze kufikiri namna nyingine ya kutatua tatizo hilo hasa

kwa kutumia njia mbadala kama vile
kufanya usindikaji wa zao lake.

MIKATABA YA UNUNUZI

Mbali na upatikanaji wa taarifa za masoko
kwa wakulima wa bustani, ni muhimu pia
wakulima kuhakikisha kunakuwapo
mikataba inayoeleweka baina yao na
wanunuzi.

Mikataba hii itawawezesha kujua
wanazalisha nini, watapata huduma wapi,
watauzi wapi, watauzi kwa nani na
watauzi kwa bei gani. Aidha kabla
wakulima hawajaingia katika kufanya
mikataba, ni muhimu wakawa na uelewa
mkubwa wa namna ya uuzaji wa mazao
hayo ya bustani ndani ya nchi na hata nje ya
nchi, bila kudanganywa na bila kudidimizwa
ili kuendeleza uchumi wao wenyewe na wa
nchi kwa jumla.